MASSACHUSETTS
Department of
Early Education and Care

## Ahadi ya Kulala kwa Usalama ya Mhudumu wa Mtoto Ili Kupunguza Hatari ya Ugonjwa wa Kifo cha Ghafla kwa Watoto wachanga (SIDS)

Watoa huduma wote wa watoto wanaowatunza watoto wachanga lazima waahidi kwamba wanafuata kanuni, sera na taratibu za Kulala kwa Usalama za EEC kwa kila mtoto aliye chini ya umri wa miezi 12 katika malezi yao.

Yanajumuisha lakini hayajazuiliwa kwa:

**Kuzungumza kuhusu kulala kwa usalama na familia kwa:**

- Kujadili mazoea ya Kulala kwa Usalama na wazazi na kutoa taarifa za Kulala kwa Usalama;
- Kuwafahamisha wazazi kuhusu wajibu wa mpango wa kutii sera na kanuni za Kulala kwa Usalama za EEC; na
- Kuwafahamisha wazazi kuhusu taratibu za mpango iwapo hali ya dharura itatokea.

**Kufanya kulala kuwa wakati salama kwa:**

- Kuwalaza chali watoto wachanga wote walio chini ya miezi 12;[1]
- Daima kuwaweka watoto wachanga kwenye kitanda chao cha kulala (wasilale kamwe kwenye kitanda chako, kiti cha gari, kibembea, kitanda cha mtoto kinachobembea, sofa, au kiti) ambacho hakina vitu vya kuchezea, wanyama serere waliojaa, na matandiko laini;
- Usiwahi kufunika kichwa cha mtoto mchanga;
- Kuwaweka watoto wote wanaolala mahali ambapo wanaweza kusikika na kuangaliwa mara kwa mara wanapolala; (Kumbuka: watoto wote wachanga waliojiandikisha katika mpango wa malezi ya watoto walio na umri wa chini ya miezi 6 lazima wawe chini ya uangalizi wa moja kwa moja kila wakati kwa muda wa wiki sita za kwanza wanapokuwa chini ya malezi)
- Kuweka joto la kawaida la chumba (kati ya farenhaiti digrii 68-72); na
- Kutokuwa na moshi katika mazingira ya kulala.

**Iwapo kuna hali ya dharura itatokea:**

- Tutapiga simu kwa 911 mara moja.
- Hakikisha kuwa angalau mtu mmoja aliye na cheti cha sasa cha CPR na Msaada wa Kwanza yuko kwenye majengo wakati watoto wapo.

**Ninaelewa kuwa EEC inaweza kuchukua hatua za haraka na muhimu ikiwa ukiukaji wowote zaidi unaohusiana na Kulala kwa Usalama utapatikana kwenye mpango wangu wa malezi ya watoto, ikiwemo kusimamisha uandikishaji wa watoto wachanga, kubatilisha, kusimamisha, na/au kukataa kufanya upya leseni ya mpango wangu.**

| | |
|---|---|
| Saini ya Mwenye Leseni au Mwakilishi | Tarehe |

[1] Isipokuwa kama daktari wa watoto ameshauri nafasi mbadala ya kulala kwa maandishi, au mtoto anaweza kujigeuza mwenyewe na walikuwa wamejigueza wenyewe na kulala chali.